Utangulizi :

Enyi ndugu Waislamu twamuomba Allaah atujaaliye tuwe wenye kushukuru ne'ma zake, na tuwe wenye subra wakati wa mitihani na misukosuko. Kwa hakika kumetokea katika wakati wetu huu fitna nyingi – ambazo hubadilisha hali za ki maisha na kuleta ufisadi mkubwa , na kuleta ikhtilaafu za mioyo yetu, na kuzinduhsa bid'ah, na kuipinga Sunnah : ambayo mambo yote haya ni dalili katika kukaribia mwisho wa dunia na kuja Qiyama.

Na katika balaa hizi zilizokuja na kuwa mtihani kwa Waislamu wengi –hususwan vijana- , ni kutokeza kwa yule anaitwa Usaamah bin Laadin.

Ambaye amejitweka katika mambo magumu na katika upotefu wa kuhuisha bid'ah ya ki khawaarij – hali ya kuificha na kuwa akitangaza kuwa hiyo ndiyo Da'wah as-Salafiyyah halisi ! Pamoja na kuleta mfarikano na kudhoofisha Shariah kwa kufanya ugaidi dhidi ya Mamlaka Ya Saudia, na Nchi nyengine za kiislaamu – kwa jina la jihaad!

Alhamdulillaah kwa kuwekelea katika Ummah huu ; Ulamaa wenye juhudi nyingi, ambao wame wafikiwa kumtambuwa mtu huyu , na kufichuwa siri zake, na kubainisha ukweli wa hali yake.

Lakini vile vile bado wako wale wenye kuita watu na kuwatia katika baatil – hao bado wanajaribu kuficha kauli hizo , na fatwa hizo za Ulamaa kuhusu upotofu wa Usaamah bin Ladin na kipote chake.
Lakini , Haki haifichiki Abadan. Na Allaah amekataa kuistawisha baatil :

بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ

"Bali tunaitupa haki juu ya uwongo ; na ikauvunja na mara (baatil) iukatoweka (ikaondoka)…" [1]

Basi , Ewe Ndugu mpendwa, Hizi fatwaa mbele yake zisome na uzisambaze.

Ubainifu wa usalama na unadhifu wa Manhaj ya Salaf utambulike, na ijulikane kuwa watu wa haki – watu wa Firqatu Naajiyah [kipote kilicho okoka] – wako mbali na ufisadi wa ma khawaarij.

Wa billaahi Tawfeeq :

[1] Suraatul Anbiyaa :18

Al-Imaam Al-Mujaddid Shaykh Abdulazeez Ibn Baaz (Rahimahullaah) :

Alisema katika Jarida la Buhooth al-Islaamiyya , nambari 50 , kurasa 7-17 :

"..Ama haya ambayo wako nayo hivi sasa Muhammad al-Mas'ari na Sa'd al-Faqih [2] na wenzawo – katika mambo ya kutangaza Da'wah za ufisadi na upotofu : basi hapana shaka kuwa hii ni shari kubwa. Nao wao ni walinganizi wa shari kubwa, na ufisadi mkubwa.

Na ni wajibu kutahadharisha na ulinganizi wao , na kuubatilisha, na kutowasaidia katika kitu chochote chao ambacho kina lingania katika ufisadi na baatil na shari na fitna.

Kwa sababu Allaah ame amrisha kusaidiana katika kumcha Yeye na katika mambo mema, wala tusisaidiane katika ufisadi na shari na kutangaza uwongo , na kutangaza Da'wah za baatil ambazo zina sababisha mfarakano na kukoseka kwa amani , na mambo mengine..

Kwa hivyo haya matangazo yanayo toka kwa faqih au mas'ari au wengineweo katika walinganizi wa baatil , na walinganizi wa shari na mfarakano : ni lazima kuzikataa na kuziharibu , na kutozikubali. Na ni lazima kuwapa naswiha na kuwalingania katika haki, na kuwaonya na upotofu. Na wala haifai kwa mtu yeyote kulingana nao katika hii shari, na ni lazima wapewe naswaha, na waregee katika mwenendo wa sawa , na wawache huu upotofu.

Nasiha yangu kwa mas'ari na faqih **na bin ladin** na wote wenye kushika njia yao : ni wawache hii njia chafu, na wamche Allaah, na waogope adhabu yake na ghadhabu yake, na waregee katika njia ya sawa, na watubie kwa Allaah kwa yale yaliyopita.

Na hakika Allaah amewapa ahadi waja wake wenye kutubia kuwa tauba zao zitakubaliwa, kama alivyosema Allaah Subhanahu :

[2] Hawa wawili walikuwa katika wale waliodai wanataka kuleta mabadiliko katika uongozi wa mamlaka ya kiislaamu ya Saudia ; walete uchaguzi ! Walipobainisha fikra zao za kikhawaarij za kupiga vita uongozi wa kiislaamu ; walikimbia na kwenda Uingereza. Wakawa wanatowa vikaratasi mara baada ya mara kuleta fitna na pia kufanya maandamano huko Uingereza !

قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَى أَنْفُسِهِمْ لا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ *

وَأَنِيبُوا إِلَى رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ ثُمَّ لا تُنْصَرُونَ

" Sema : Enyi waja wangu mulio jidhulumu nafsi zenu! Msikate tamaa na rehema ya Allaah. Hakika Allaah husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.

Na rejeeni kwa Mola wenu , na silimuni [na kunyenyekea] kwake, kabla ya kukujieni adhabu. Kisha hapo hamtanusuriwa." [3]

Na Pia Alisema Allaah Subhanahu :

وَتُوبُوا إِلَى اللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَا الْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ

"..Na tubuni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waumini, ili mpate kufanikiwa. " [4]

Fatwa ya pili ya al-Allaamah Al-Imaam Ibn Baaz (rahimahullaah):

Katika jarida la 'al-Muslimun ' : toleo la tarehe 9 Jamadul-Uula , mwaka 1417 :

Alisema al-Imaam Ibn Baaz kuwa Usaamah ibn Laadin ni katika *al-mufsideena fil ardh* [wenye kuleta ufisadi katika ardhi] , na yupo katika njia ya ufisadi na shari , na ametoka katika [usawa na aqeedah swahihi] ya kuwatwii viongozi.

[3] Suraatul Zumar : 53-54

[4] Suraatul Nur : 31

Shaykh Al-Allaamah Swaaleh ibn Fawzaan al-Fawzaan (hafidhahullaah):

Walitokea watu wengine ambao walikataa Fatwa ya Al-Imaam Ibn Baaz aliyotowa dhidi ya bin Laadin , bali hawakusimama hapo ; wakendelea kumsifu bin laadin.

Hivyo akaulizwa Sheikh Fawzaan kuhusu hilo , na kuwa [pia wanasema kuwa] Shaykh Bin Baaz hakuzungumza kumpinga bin laadin , na kuwa fatwa hiyo inayo nasibishwa na Shaykh Bin Baaz ni uwongo.

[Na akaambiwa Sheikh Fawzaan kuwa pia] Na wako watu wengi wanatumia maneno haya [na kumtetea bin Laadin]?

Akajibu Sheikh :

“ Mwenye kusema kuwa Fatwa ya Sheikh Ibn Baaz aliyotowa dhidi ya bin Laadin ni uwongo : basi yeye [mwenye kukataa fatwa hiyo, yeye] ndiye muwongo !

Hakika fatwa hiyo si uwongo.

Sisi tuliisikia fatwa hiyo kutoka kwa Sheikh. Sisi tuliisikia kutoka kwa Sheikh.

Na imeaandikwa katika fatwa zake, na akasomewa [fatwa hio] alipokuwa hai .

Na alipo kufa ilisomwa mbele ya masheikhe na wakaikubali.

Hivyo mwenye kusema kuwa Fatwa ni uwongo : basi yeye ndiye muwongo !” [5]

Suala :

“ Si siri kwa Shaykh kwa tendo la Usama bin Ladin kutia hamasa vijana katika ulimwengu mzima , na [tendo lake la] kuleta ufisadi katika ardhi.

Jee inafaa kwetu sasa kumpa yeye sifa ya kuwa ni Khawaarij? Na hususwan pia kwa sababu yeye anasaidia kujilepua katika miji yetu na mengineo? ’’

[5] Inapatikana hapa : http://www.alfawzan.ws/AlFawzan/sounds/00233-04.ra . Na hizi fatwa zote za sheikh fawzaan zipo kwenye huo mtandao wake.

Akajibu Shaykh :

" Yeyote mwenye kubeba fikra hizi ; basi yeye ni Khawaarij. Yeyote mwenye kubeba fikra hizi, na kuita watu kuingia katika fikra hizo, na akahimiza watu katika hilo ; basi yeye ni Khawaarij. Na hii inajulikana kwa kuangalia majina yao na mahali pao.

Kwa hivyo huu ndio msingi –kuwa kila mwenye kulingania watu katika fikra hizi , na kuwapiga vita viongozi wa kiislaamu, na kuwa kufurisha waaislaamu, na kufanya halali damu za waislaamu : basi huyu ni Khawaarij. "

Suali hili linauliza :

'Sheikh , kwa nini hakujatoka fatwaa kutoka kwa *Haiyya Kibaar al-Ulamaa* [kamati ya Ulamaa wakubwa] kutahadharisha kutokana na kiongozi wa khawaarij kama vile bin Laadin, na dhawaahiri , na faqih : ili wasije wakadanganyika nao watu wengi , hususwan vijana?'

Akajibu Shaykh :

" Imetoka kwa *Haiyya Kibaar al-Ulamaa* [kamati ya Ulamaa wakubwa] onyo kutokana na amali hizi na watu wake - zimetoka onyo kadha , kwa mara baada ya mara. Zimetoka onyo kuhusu hio, na pia kwa kila mwenye kuwasaidia , hakika anaigia katika onyo hio pia."

Shaykh Al-Muhaddith Muqbil ibn Haadi al-Waadi' (rahimahullaah) :

Katika kikao na jarida *"ar-Ra'yy al-'aam"* la kutoka Kuwait , nambari : 11503 , toleo la tarehe 1998/12/19. Alisema Shaykh Muqbil (rahimahullaah) :

" Najiweka mbali mbele ya Allaah kutokana na Bin Laadin. Hakika yeye ni msiba mkubwa , na ni balaa kwa Ummah, na vitendo vyake ni shari [tupu]. "

Katika kikao hicho hicho akaulizwa Shaykh :

Kuhusu kuwa waislaamu wana lekezewa shida na dhiki katika miji yasiyo ya kiislaamu – kwa sababu ya haya matokeo ya malipuko – hata yakiwa mahali popote ?

Akajibu Shaykh Muqbil (rahimahullaah) :

" Mimi najuwa hilo. Na wame nizungumzia ndugu zetu kutoka Uingereza wakishtaki dhiki wanayopata, na wakaniuliza jee yafaa kutangaza kuwa tuko mbali na Usaama Bin Laadin?

Tukawajibu kuwa sisi tumejiweka mbali naye na vitendo vyake kutoka zamani sana.

Na haya matokeo ya sasa yanashuhudia kuwa Waislaamu wana elekezewa shida na dhiki , kwa sababu ya vitendo vya harakati za Ikhwaanil Muflisin , na wenginewo.

Na hakika usaidizi unatuko kwa Allaah."

Suala :

"Jee mulitanguliza naswaha kwa Usaama Bin Laadin?"

Akajibu Shaykh Muqbil (rahimahullaah) :

" Hakika nilituma naswiha , lakini Allaah anajuwa zaidi ikiwa ilifika ama laa. Na walitujia ndugu kutokana nao [kina bin Laadin] wakitusaidia na kushirikiana nasi katika kulingania katika njia ya Allaa. Na baada ya hapo wakaja na mali na wakatuuliza na kutuomba tuigawanye baina ya viongozi wa makabila ; ili wapate kutetewa na wanunuwe silaha – lakini nilikataa hivo. Na nikawaambia wasije tena mara nyingine katika nyumba yangu. Na nikawabainishia kuwa kazi yetu ni Da'wah pekee, wala hatukubalii wanafunzi kuiingilia mambo mengine [pasi na Da'waah]."

al-Allaamah sheikh Ahmad an-Najmee (rahimahullaah) :

…Baada ya kubainisha dalili za Aya na hadithi kuhusiana na uwazi na usalama wa Uislaamu [asili] na kuhusu upotofu wa khawaarij … alisema sheikhe.. [6]

" …Basi pamoja na hayo, ni maalumu kuwa Uislaamu uko mbali na haya mambo ya ufisadi na ya kiwazimu , na uhakika ni kuwa mambo haya hukatazwa, na hupingwa anaye yafanya , na mambo haya humtokomeza mwenye kuyafanya.

Hakika wenye kuwa singizia Salafiyyun –ambao wanafwata Kitabu cha Allaah , na Sunnah Ya Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam , kwa ufahamu wa Maswahaba - kuwa ati wao ndio wenye kufanya mambo haya ya kujilepua huko Uingereza na kwengineko, ambayo ni mambo ya kuuwa nafsi, na kuharibu mali, na kumwaga damu, na kuleta khofu kwa watu :

Hakika mwenye kuwasingizia watu wa Manhaj ya Salaf ati ndio wenye kufanya munkar (madhambi makubwa) hayo : kwa hakika wao ndio wenye kuyafanya mambo hayo lakini wanataka kuwasingizia wengine. !!

Wao ni watu wa kundi la Al-Qaida ambao ni wafuasi wa Usama bin Ladin , na Mus'ari, na Faqih , na wenzao.

[wao wanafanya hivo] Sababu wao wame kuzwa katika vitabu vya watu wenye kufanya takfir [kukufurisha waislaamu] kama vile Sayyid Qutb na ambao wako naye katika huu mfumo wa makosa – ambapo wana wakufurisha Ummati Muhammad sallahAllaahu alayhi wasallam bila ya haki….. ''

[6] Makala hii aliandika sheikh chini ya anwani : 'Salafiyyin wanajiweka mbali na watu wa Ugaidi.' Inapatikana hapa : http://www.dar-ketabsunah.com/monthly_article/Annajmy01.html

Shaykh Al-Allaamah Swaaleh ibn Muhammad al-Luhaydaan (hafidhahullaah):

Suala :

‘ Ni nini msimamo gani [unaotakikana] kwa muislaamu kuhusu kundi la Al-Qaida na mfumo wao unaosimamishwa na Usaama Bin Laadin?’

Akajibu Shaykh :

“ Hapana shaka kuwa kundi hilo halina khayri ndani yake, na wala si katika njia za kuleta islaah [marekebisho].

Na hakika mfarakano wa waislaamu na kupatika makundi yaliyo tofauti na yaliyovunjika: ni katika sababu za balaa na shari, na ni katika mambo ya mfarakano , na yanaleta umwaganyi wa damu….”’

Mpaka mwisho wa maneno yake .. yanayopatikana hapa :

http://www.alnawader.net/nawader_v/fatawe/listen/lu7idan-alqa3edah.ram

Dkt. Ibraahim ibn Abdullaah al-Mutlaq (hafidhahullaah)

Aliandika makala katika Jarida la Riyadh : Siku ya alkhamisi 26 Rajab 1428 , nambari 14290. Anwani yake ilikuwa ni :

Ibn Laadin ni Imaam wa Khawaarij , si Imaam wa Mujaahidin !

Alisema sheikh Ibraahim hafidhahullaah :

“Wana sema baadhi ya watu ambao wame hadaika na sheikhe wa khawaarij na imaamu wao : Usamaah bin Laadin – kuwa yeye ni Imaam wa Mujaahidin, na sheikhe wa jeshi !!

Na hapana shaka kuwa huyu hastahiki taji hilo, wala yeye si mtu anayefika daraja hio. Na kwa uhakika yeye anastahiki kuwa yeye ni Imaam wa Khawaarij wa wakati huu.

Kwa hakika ameleta mfarakano, na aka kufurisha waislaamu wenye kumuabudu Allaah pekee ; katika viongozi na wanachuoni, na hususwan viongozi na Ulamaa wa nchi hii tukufu [Saudi Arabia] – ambao wao ndio waliokaribu zaidi na msimamo wa sawa, na kuleta marekebisho ya ndani na ya nje , na ndio watu wenye ukweli zaidi katika kumtwii Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam , na ndio watu wanao shikamana zaidi na Kitabu cha Allaah na Sunnah na kutekeleza hukmu zake.

Vipi atakuwa bin laadin ni Mujaahid hali ya kuwa amepiga vita viongozi wa kiislaamu na akawacha baya’ yake, na akamkufurisha ?

Na vipi atakauwa yeye ni Mujaahid ; hali ya kuwa amemzushia na kumtukana Al-Imaam Shaykh Ibn Baaz (rahimahullaah) ?

Na vipi atakauwa yeye ni Mujaahid ; hali ya kuwa ame khalifu hukmu za Jihaad ambazo zimebainishwa na wanvyuoni wa kale (Salaf) , na zika sisitizwa na wanavyuoni wachaMungu wa wakati huu ?..

Kisha akaendelea kusema sheikh:

“ Ni jihaad gani anaypigania huyu mbeba bendera ya khawaarij : ambaye amekhalifu kila hukmu ya jihaad iliyokuja katika Kitaabu cha Allaah na Sunnah ya Mtume wake sallahAllaahu alayhi wasallam ?

Ni jihaad gani anayopigania huyu mbeba bendera ya khawaarij : ambayo anasisitiza kwa wale anawo wachukuwa kupigana, kuwa : jihadi hii ni lazima kwa kila mtu, na ni lazima hata wakate kizazi na kutowasikiza wazee wao ; ili wajiunge naye?..”

Huu ni ufupisho wa maneno marefu aliyo andika sheikhe.

Mukhtasar :

Alhamdulillaah , tunataraji baada ya makala hii kuwa ndugu zetu wamejuwa ukweli na ubainifu wa msima wa Ulamaa na watu wa Sunnaah kuhusu bin laadin na kikundi chake.

Kwa hakika marekebisho na utawala kwa Uislaamu hauji kwa fujo , wala dhambi, wala mfarakano, wala ujaahil.

Hakika alisema ukweli Imaam Maalik (rahimahullaah) :

" Ummah huu hautosuluhika ila kwa kutumia mbinu ile ile iliyo suluhisha karne za kwanza.. "

Nayo ni kupitia kufwata Kitabu cha Allaah , na Sunnah Ya Mtume sallahAllaahu alayhi wasallam , kwa ufahamu wa Maswahaba : kama inavyotakikana. Bila ya uzushi wala upungufu.

Amesema Allaah Subhanahu :

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُم فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُوْلَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

" Allaah amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyo wafanya makhalifa waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi [Allaah], wala hawanishirikishe na chochote. Na watakao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri zetu.

Na simamisheni Sala, na toeni Zaka, na mt'iini Mtume, ili mpate kurehemewa."

Suratu Nur : 55-56

Alhamdulillaah Rabil Aa'lameen.